**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA**

**KIDATO CHA PILI 2024**

**1.INSHA.**

Hii ni insha ya barua rasmi.Vipengele muhimu vya insha ya aina hii viweze kujitokeza.

Vipengele hivi ni:

a.Muundo /sura

Sura ya barua rasmi ijitokeze.

Vipengele vifuatavyo vijitokeze.

i)Anwani mbili.

ii)Tarehe

iii)mtajo

iv)KUHUSU-mada ya barua iandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari.

v)Hitimisho.

*Tanbihi.*

*Baadhi ya hoja za kushughulikiwa ni kama.*

i)Matumizi ya dawa za kulevya.

ii)Shinikizo la rika.

iii)Ukali wa waalimu.

iv)Kusongwa na mawazo ya uharibifu.

v)Hamu ya kurundi nyumbani kutokana na shughuli nyingi shuleni.

vi)Ukosefu wa ushauri nasaha shuleni.

## 2. UFAHAMU

A i) Ucheleweshaji wa utoaji wa vitambulisho vya kitaifa.

ii)Huduma za mateso katika hospitali za umma.

iii)Watu waliostaafu kufariki bila kulipwa malipo yao ya uzeeni.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

B)i)Wafanyakazi wa serikali huwa wanahangaishwa.

ii)Kuwatesa.

iii)Kuwakosea heshima wanaofika katika ofisi zao kutafuta huduma. (alama3x1=3)

C)i Kutelekezwa kwa wagonjwa.

ii Wodi zenye misongamano ya watu.

iii)Vyumba ambavyo havina mwanga. (alama 3x1=3)

D)Serikali inafaa kuzinduka na kufanya mageuzi kamilifu. (alama 2x1=2)

E)i Kujitolea kwa yakini kuwashughulikia raia.

ii Kuwakomboa kutokana na manyanyaso wanaopitia mikononi mwa watesi hawa wanaojiita watumishi wa umma. (alama 2x1=2)

F) Asasi nyingi za serikali zina sifa mbaya machoni pa wakenya. (alama 1x1=1)

G) i.Ushuru-Ada ya lazima au ada ya kifedha inayotozwa na serikali yoyote kwa mtu binafsi au shirika ili kukusanya mapato ya kazi za umma zinazotoa vifaa na miundombinu bora zaidi.

ii. Uwezo (alama 2x1=2)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Irabu /o/

Juu

Nyuma

Viringwa **zozote mbili** (alama 2x1=2)

b) kijana –kivumishi nomino

hiki –kivumishi kionyeshi. (alama 2x1=2)

c) ‘Kunywa (alama 1x1=1)

d)Nyoka ambaye alimuuma ameuawa.

Au



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Nyoka aliyemuuma ameuawa. (alama 2x1=2)

e)Mabuzi hayo yatanunuliwa kesho. (alama 2x1=2)

f)i Hali ya –me

ii.Hali ya hu-

iii) Wakati uliopita. (alama 3x1=3)

g)Askari alisema kuwa wangemtia baroni mhalifu huyo wakati huo.

(alama 3x1=3)

h )Wa-nafsi ya tatu wingi

li-wakati uliopita

som-shina/mzizi wa kitenzi

eshw-kauli/mnyambuliko wa kitenzi kauli ya tendeshwa

a –kiishio

je-kiabishi tamati kiuulizi. (alama 6x1/2=3)

i)Mama alianika nguo kisha akaepua chungu jikoni.

j) i Kijana amefika.

ii Mwalimu kijana anafunza (alama 2x1=2)

k) i Kuandika saa mfano 4:30 Asubuhi

ii Kutenga shilingi na senti mfano bei ya mafuta ni 196:20

iii) Katikia kuandika diolojia mfano

Sudi:

Ashua: (alama 3x1=3)

l) Watalii huvutiwa na Mlima Kenya. (alama 1x1=1)

m) yuyu huyu –kiwakilishi kisisitizi

***a*** (liwatembelea)-kiwakilishi cha nafsi kiambata/kitegemezi (alama 2x1=2)

n) Jitu- LI/YA

Kitukuu-A/WA



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

o) Mwizi hakuiba kikapu wala ng'ombe. (alama 2x1=2)

p)Msafara/mlolongo

Kikosi (alama 2x1=2)

q)Mama aliandika barua ipelekwe,ipokelewe au kuelekea kwa baba.

Mama aliandika barua kwa niaba ya baba. (alama 2x1=2)

r) M-Wa Mtu -Watu

Ch-Vy Chura-vyura

Ki-Vi kiwete –Viwete yoyote miwili (alama 2x1=2)

s ) hufunzwa an ulimwengu. (alama 1x1=1)

*(adumishe maneno halisi ya methali)*

t) bibi-mke wa mtu

-nyanya (alama 2x1=2)

**4. ISIMU JAMII**

i) Sajili ya Posta (alama 2x1=2)

ii) Sifa za sajili ya posta

i) Msamiati maalum kama vile barua,simu,kutuma barua,stempu NK

ii)Kauli Fupi Fupi hutumika.

iii)Lugha yenye adabu na heshima hutumika.

iv)Lugha rasmi.

v)Utohozi-Stempu.

vi)Lugha dadisi-Unataka kutuma barua wapi?

iii. a) Huwafunza watu kaida za lugha ili waweze kuzitumia ipasavyo kutegemea mila na desturi.

b) Humsaidia mzungumzaji au mwandishi kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na usahihi.

c) Humpa anayetambua lugha uwezo wa kutambua,kutofautisha na kutumia miundo mbalimbali ya lugha kutegemea mahitaji.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

d)Hufunza maadili ya jamii hasa yanayohusiana na matumizi ya lugha kutegemea uhusiano.

e)Hufunza mbinu za mawasiliano pamoja na mbinu za kupata maana kamili.

f) Hudhihilisha utamaduni wa jamii. za kwanza nne (alama 4x1=4)

**5. FASIHI SIMULIZI**

a i ) Hekaya-Hadith ya zamani ambayo inaaminika na watu wengi lakini haiwezi kuthibitishwa kuwa ya kweli ambayo inakiwango fulani cha ujanja/udanganyifu/ulaghai.

ii) Mandhari-mazingira ambapo kazi ya fasihi inatendewa.

iii)Hurafa-hadith zinazotumia wanyama kama wahusika.

(alama 3x1=3)

b) Sifa za vitendawili.

i) Huwa vifupi kimaelezo

ii) Hutumia lugha ya kimafumbo.

iii) Hutolewa mbele ya hadhira.

iv) Hutumia ufananisho wa kijazanda.

v) Hutumia ufananisho wa kijazada.

vi) Huwa na wakati maalum wa kutolewa yaani jioni.

vii)Huweza kuwa na fomyula/muundo maalum.

Mtegaji:Kitendawili

Mteguaji:Tega za kwanza nne (4x1=4)

c) Jadili sifa nne za mtambaji bora.

i)Mbunifu – awe na uwezo wa kuwasilisha hadithi kwa namna ya kuwachangamsha. Abuni hadithi upya mara tu anapoitamba.

ii)Afahamu lugha- Awe na ufahamu mpana wa lugha husika na utamaduni unaohusika ili awasilishe vyema ngano yake.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

iii)Afahamu hadhira yake na mahitaji yao- wake , waume, watoto, vijana, nk . apatane vyema na mazingira yake ya kisimulizi.

iv)Mcheshi- ili kuinasa makini ya hadhira yake.

v) Uwezo wa ufaraguzi na afahamu mbinu zifaazo za sanaa na maonyesho – uwezo wa kuunda, kugeuza na kuwasilisha kazi ya fasihi simulizi papo hapo.

vi)Afahamu tabia za binadamu- mambo yanayofurahisha, kuudhi, kuchangamsha, kuvutia au kumpendeza. Pia wafahamu mikondo mbalimbali ya jamii.

vii)Sauti yake isikike na ibadilike ipasavyo.

viii)Ashirikishe hadhira yake- anaweza kuwauliza maswali, waimbe nyimbo nk

ix)Jasiri – aweze kuzungumza hadharani bila haya hasa masuala ya aibu.

x) Afahamu utamaduni wa hadhira yake ili atoe ujumbe kwa njia inayokubalika na hadhira na asije akatumia ishara au maneno yasiyokubalika pale.

za kwanza nne (alama 4x1=4)

d) **Umuhimu wa maigizo.**

i) Michezo ya kuigiza huburudisha watazamaji. Watu hutumbuizwa na kupumbazwa na maigizo kama vile ngoma za kitambuni na vichekesho.

ii)Ni kitambulisho cha jamii. Kila jamii ina sanaa yake ya maigizo ya shughuli za jamii husika.

iii)Hukuza umoja na ushirikiano. Watu wanapokuja pamoja kushiriki katika maigizo hujitambulisha kama jamii moja.

iv)Ni nyenzo ya kupitisha maarifa na amali za jamii.

v) Husawiri mitazamo ya jamii kuhusu masuala mbalimbali. Baadhi ya uigizaji hukejeli vitendo hasi vya wanajamii kama woga, wivu, chuki na usaliti.

vi)Husifu tabia chanya.

vii)Hukuza uzalendo – kupitia kwa maigizo kama vile miviga, vijana hujitambulisha na jamii zao na kuzionea fahari.

viii) Huimarisha na kupalilia ubunifu. Watoto wanaposhiriki katika michezo ya watoto hujifunza kubuni michezo wakiwa wachanga.

ix)Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Desturi za jamii kama vile upashaji tohara, matambiko, majigambo na miviga hudumisha kupitia kwa maigizo.

x) Hukuza kipawa cha uongozi. Waigizaji wanapochukua majukumu ya uongozi katika michezo huweza kujifunza stadi za uongozi.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

xi)Huelimisha kupitia kwa maudhui na hulka za waigizaji, hadhira hupata fursa ya kujitathmini na kushauri nafsi zao kuiga au kukashifu hulka hizo.

xii)Mwongoza jamii kupambana na mazingira wanamojipata. Kutegemea imani ya wanajamii matambiko yanaweza kuondoa matatizo kama vile njaa,ukame na ugonjwa kutoka katika jamii.

zozote nne ( 4 x 1 =alama 4)

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes